TOLEO LA 30
Salamu kwa Familia ya Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb,

Natumai kila mtu alikuwa na wiki yenye tija. Tunapofunga mwezi wa Machi, ninasherehekea maendeleo ambayo Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb (DCSD) imefanya ili kuhakikisha mafanikio katika kufunguliwa upya. Ninajivunia wasomi, waalimu na wafanyakazi wetu wote kwa juhudi zao katika kufanya mabadiliko ya masomo mahuluti kuwa taratibu iwezekanavyo.

Mnamo tarehe 29 Machi, tutabadilisha na kuwa na viwango vyote vya gredi (vikundi vya A na B) katika majengo ya shule kwa kipindi kinachosalia cha mwaka wa shule. Nina hakika kwamba kila mtu atachangia sehemu yake ili kufanya mabadiliko haya yajayo kuwa salama na yenye mafanikio.

## Mwongozo Mpya wa CDC

Ili kuendelea kuweka shule zetu salama na kupunguza kuenea kwa maambukizi, lazima tukumbuke kufuata miongozo kutoka kwa Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC). CDC ilisasisha mwongozo wake wa shule ya K-12 ili kujumuisha maelezo ya hivi karibuni ya sayansi kuhusu umbali wa kimwili kati ya wanafunzi madarasani. CDC sasa inapendekeza kwamba, pamoja na kila mtu kuvaa barakoa, wanafunzi wanapaswa kudumisha umbali wa angalau futi 3 katika mazingira ya darasa.

Kama ninavyosisitiza kila wakati, DCSD itafuata sayansi na kutekeleza mikakati ya kupunguza hatari—iliyopendekezwa na CDC—ili kuhakikisha kila mtu katika majengo yetu yuko salama. Tunapokaribia likizo ya msimu wa kuchipua, ningependa kuhamasisha wanafunzi, waalimu, wafanyakazi na familia zetu kuendelea kuzingatia mikakati ya kupunguza hatari wakati hatuko katika majengo. Natumai kila mtu atachangia sehemu yake ili kusaidia kuweka idadi ya maambukizi ya COVID-19 chini kwenye jamii ya Kaunti ya DeKalb.

## Chanjo ya COVID-19

Ingawa Wilaya inaendelea kuweka shule zetu salama na kupunguza kuenea kwa maambukizi kwa kufuata mwongozo wa kupunguza hatari wa CDC, DCSD pia inatoa fursa kwa wafanyakazi wetu kupata upimaji na chanjo ya COVID-19. Ninafurahi kutangaza kwamba kwa usaidizi kutoka kwa Bodi ya Afya ya Kaunti ya DeKalb (DCBOH) na washirika wengine wa afya, DCSD imewachanja wafanyakazi 1,704 tangu serikali iliporekebisha mpango wake wa utoaji wa chanjo kwa wafanyakazi wa awamu ya 1b.

Wafanyakazi wa wilaya wameweza kupokea chanjo katika Kituo cha Usimamizi na Mafundisho cha DCSD, Kanisa la St. Phillips AME na duka la dawa la Briarcliff. Wauguzi wa DCSD, ambao wamepata mafunzo, walitoa baadhi ya chanjo kwa wafanyakazi mnamo tarehe 20 Machi wakati wa tukio letu la chanjo kwenye Kituo cha Usimamizi na Mafundisho.

DCSD itaendelea kushirikiana na DCBOH, Duka la dawa la Walgreens na Briarcliff kutoa chanjo. Pia tunawahimiza wafanyakazi na wanafunzi wenye umri wa miaka 16 na zaidi

kutafuta fursa zingine za kupokea chanjo kupitia DCBOH, maduka ya dawa ya eneo au watoa huduma wao wa matibabu.

## Bonasi

Jana, Bodi ya Elimu ya Jimbo leo imeidhinisha pendekezo la Msimamizi wa Shule za Jimbo Richard Woods kwamba Georgia itumie fedha za msaada wa serikali ya nchi kutoa malipo ya bonasi ya wakati mmoja ya $1,000 kwa kila mwalimu wa shule ya umma ya K-12 na wafanyakazi wengine wa usaidizi wa elimu.

Bonasi hiyo inatolewa kwa waalimu na wafanyakazi wa usaidizi wa elimu kusaidia katika kuajiri na kudumisha wafanyakazi wenye tajriba ya juu katika nafasi hizi muhimu kama ishara ya shukrani kwa kazi na kujitolea kwao wakati wa janga la COVID-19.

DCSD inathamini wafanyakazi wake na michango yao katika kusaidia wasomi wetu. Tunatumai kuonyesha shukrani zetu kupitia usambazaji wa bonasi hizi mwezi ujao.

## Mkutano wa Mashirika ya Wakimbizi

Ningependa kuyashukuru mashirika manane ya wakimbizi ambayo ilikutana nami na timu yetu wiki iliyopita ili kujifunza kuhusu maono yetu ya kuweka DCSD katika kiwango kipya cha ubora. Hii pia ilikuwa fursa kwangu kusikiliza mawazo, mapendekezo, matumaini na mahitaji ya jamii hii ya kipekee inayohudumia Familia zetu mpya za Marekani.

Washikadau wetu ni muhimu kwa utendaji mzuri wa wilaya yetu ya shule. Njia wazi za mawasiliano ni lazima. Kukaribisha na kukubali ushiriki wa washikadau ni lazima. Ili kujenga jamii ya uaminifu, tunaahidi uwazi wetu, na miundombinu ya kuwa washirika wazuri kwa washirika wa nje ambao wanashiriki kujitolea kwetu katika kufaulu kwa mwanafunzi.

## Mpango wa Masomo ya Msimu wa Kiangazi wa MOSAIC

Kama nilivyosema katika jarida la wiki iliyopita, DCSD itatoa Mpango wa Masomo ya Msimu wa Kiangazi wa MOSAIC kwa wanafunzi katika msimu huu wa kiangazi. Mipango ya Masomo ya Msimu wa Kiangazi ya MOSAIC inasaidia msingi wa mafundisho wa wilaya ya shule—wanafunzi wetu, waalimu wetu, na maudhui yanayofundishwa na wanayojifunza—kwa njia ya urekebishaji, kuongeza kasi, uboreshaji na ujifunzaji wa kijamii na kihisia. Lengo letu ni kuwashirikisha wanafunzi wote ikiwa ni pamoja na wanafunzi wa Kiingereza, wanafunzi wenye ulemavu, na wanafunzi wenye vipawa.

| MPANGO | HADHIRA | TAREHE ZA MPANGO | MUUNDO |
|---|---|---|---|
| Urejeshaji Alama wa FLEX | Wanafunzi wa Gredi ya 8 wanaofanya kozi za HS pekee na Wanafunzi wa Gredi za 9-12 | Juni 1 – Juni 17 | Mtandaoni katika Wilaya Yote |
| Darasa za Kwanza za FLEX | Wanafunzi wa Mwaka wa Mwisho | Juni 1 – Juni 24 | Mtandaoni katika Wilaya Yote |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ufidiaji wa Alama wa Shule ya Upili | Wanafunzi wa Gredi ya 8 wanaofanya kozi za HS pekee na Wanafunzi wa Gredi za 9-12 | Juni 1 – Juni 30 (Inategemea) | Mahuluti katika Shule ya Eneo |
| Kambi ya Mpito Kati ya Shule ya Upili na Chuo kwa AP | Gredi 9-12 | Wiki ya 1 katika Julai | Mahuluti katika Shule ya Eneo |
| Kambi ya Mpito Kati ya Shule ya Upili na Chuo ya Msimu wa Kiangazi | Wanafunzi wanaokamilisha gredi za 6 na 9 | Julai (Inategemea) | Mahuluti katika Shule ya Eneo |
| Mwaka Ulioongezwa kwa Elimu Maalum | Wanafunzi wa Elimu Maalum (Pre-K-12) | Juni 7 – Julai 16 | Mahuluti katika Wilaya Yote |
| Mpango wa Chuo cha Wasomi (Scholars Academy) | Gredi 3-8 | Juni 7 – Julai 16 | Mahuluti katika Shule ya Eneo |
| Serendipity | Gredi 1-6 | Juni | Mtandaoni katika Wilaya Yote |
| Mipango ya Uboreshaji katika Shule za Title I | Masomo ya Gredi K-12 | Julai | Mahuluti katika Shule ya Eneo |
| Kambi ya Ujuzi wa Kusoma na Kuandika | Gredi K-12 | Juni 7 – Juni 30 | Mahuluti katika Shule ya Eneo |
| Mpango wa My Brother's Keeper | Wasomi Wanaofadhiliwa na MBK | Juni 28 – Julai 2, 2021 | Mahuluti katika Wilaya Yote |
| Kambi ya Ufundi wa Vyombo vya Hewa | Gredi 4-6 | Juni 21 – Julai 2, 2021 | Mahuluti katika Wilaya Yote |
| STEM pamoja na Ujuzi wa Kusoma na Kuandika | Gredi 6-8 | Julai 19 – Julai 29, 2021 | Mahuluti |
| Mpango wa Uboreshaji wa CTAE | Inategemea | Juni/Julai | Mahuluti |
| Masomo (Uboreshaji wa Ujuzi wa Kusoma na Kuandika) | Gredi za Pre-K hadi 2 | Juni – Julai | Nyumbani |

Kanusho: Fursa za masomo za msimu wa kiangazi kwa uboreshaji, urekebishaji, urejeshwaji wa alama, na maendeleo ya kasi zaidi hutegemea mwongozo wa hivi karibuni wa jimbo, eneo na wilaya unaohusiana na ushauri wa afya wa COVID-19. Tarehe zinaweza kubadilika.

Vidokezo:

- Mipango ya ana kwa ana itawezeshwa kupitia vikundi vidogo vyenye uwiano wa mwanafunzi na mwalimu wa 1:15.
- Mipango mahuluti itajumuisha vikao vya mtandaoni na vya ana kwa ana.

**Ilisasishwa: Tarehe 26 Machi 2021**

Kupitia masomo ya ana kwa ana, mahuluti na ya mtandaoni, wanafunzi watafaidika na mafundisho yanayoongozwa na mwalimu na masomo yaliyoelekezwa na wanafunzi ambayo ni ya kukusudia. Wanafunzi watashiriki katika hali halisi, jumuishi na muhimu.

Maelezo ya usajili kwa mpango wa msimu wa kiangazi yatatolewa tarehe 19 Aprili 2021.

## Mwaka wa Shule wa 2021-2022

Huku Wilaya ikifanya mipango ya mwaka wa shule wa 2021-2022, tunazingatia mahitaji ya kimasomo, kijamii, kihisia na kitabia ya wanafunzi wetu. Ni muhimu tuendelee kuzingatia matokeo ya wanafunzi na kupanga kuhusu chaguo za masomo ya ana kwa ana kwa mwaka ujao. Tunapanua pia Chuo cha FLEX ili kutoa masomo ya mtandaoni kama chaguo kwa wanafunzi wa shule ya kati na sekondari. Iwapo familia inachagua masomo ya mtandaoni, tungependa kuhakikisha kuwa wanafunzi wanashiriki kikamilifu katika masomo

yanayoongozwa na mwalimu (mafundisho ya moja kwa moja yanayoongozwa na mwalimu) na masomo ya kujiongoza mwenyewe (mafundisho ya mtandaoni yasiyoongozwa moja kwa moja na mwalimu).

Wilaya itaandaa mikutano ya maelezo mnamo Aprili ili kukusanya maoni yako tunapopanga mwaka ujao.

Mpango wa Kids'-Doc-On-Wheels/Siku ya Kuwa Nje

Nilipata fursa ya kukutana na Dk. Lynette Wilson-Phillips wa mpango wa Kids'-Doc-On-Wheels na timu yake katika Shule ya Msingi ya Fairington leo. Wito wa Kids'-Doc-On-Wheels, Inc ni kuhakikisha upatikanaji zaidi wa huduma bora na utunzaji wa kina wa watoto katika jamii za watoto na vile vile eneo lao la msingi la kila siku-shule. Tunashukuru mpango wa Kids'-Doc-On-Wheels kwa ushirikiano wake! Muundo wao wa tiba ya mbali husaidia kuwaweka wasomi wetu shuleni wakiwa na afya na tayari kufanikiwa!

Pia nilikuwa na fursa ya kukaa na kufuatilia madarasa machache yakiendelea katika Fairington. Nilifurahi kuona jinsi walimu na wanafunzi walivyokuwa wanashiriki. Ningepedna kumshukuru Mwalimu Mkuu Dkt.Walter Burke kwa kunikaribisha kwenye jengo lake. Ninataka pia kumshukuru Msimamizi wa Eneo Dk Triscilla Weaver kwa kujitolea kwake katika kuwasaidia wasomi wetu.

Tafadhali endeleeni kujilinda wenyewe na wengine.

Wako mwaminifu,

Bi. Cheryl Watson-Harris